JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI

DUNIA BADO IKO KWENYE HATARI

Dunia bado iko kwenye hatari, hayo yamesemwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Fedha la Kimataifa Bw. Dominique Strauss-Kahn alipokuwa akizingumza na waandishi wa habari mjini hapa.

Bw. Dominique aliwaelezea waandishi hao kuwa "nisingependa watu wengi waweke kwenye mawazo yao kuwa mtikisiko sasa umepita, tunapaswa tujue kuwa bado kuna mambo yanayotuzingira hata kama tutaendelea na biashara kama kawaida. Tunapaswa kujua ni jinsi gani tutazuia hii hali ya mtikisio isitokee tena".alionya Mkurugenzi huyo.

Aliendelea kuongeza kuwa "Kama wote mnavyofahamu , uchumi umerudi katika hali yake kuliko tulivyotegemea.Tunategemea katika mwaka ujao uchumi wa Dunia kukua kwa asilimia 4.2, zaidi ya tulichokisema miezi sita iliyopita. Hili ni agano ambalo limetimilika bila kutegemea katika sera za ujumla tulizojiwekea, "nataka niwakumbushe kuwa Shirika la Fedha la kimataifa linasema kuwa utaratibu huu utazaa matunda na ndicho kitu ambacho kinafanyika.Kitu cha kwanza ninachopenda niwaambie ni kwamba, ushirikiano huu wa kidunia umekuwa na mafanikio na hichi ndicho kitu tulichokuwa tukikitaka mwaka mmoja uliopita. kama wengine mlikuwepo mtakumbuka".

Sasa lengo letu ni nini, Lengo letu sasa ni kuulinda na kuuimarisha uchumi, kwasababu hata kama kukua huko ni imara na kumekuwa kwa haraka kuliko tulivyotegeme, unaweza ukabadilika. Unabadilika kwa sababu hautabiriki. Mmeshaelezwa kuhusu hili; suala hili mmeshaelezewa sana , nafikiri Bw. Olivier Blanchard aliwaeleza jana. Kwa hiyo sina sababu ya kusema zaidi.Alisema Dominique.

"Wote mnajua kuwa katika uchumi unaokuwa ukosefu wa ajira uko juu sana na katika nchi nyingine unazidi kuongezeka, na mahitaji binafsi bado ni dhaifu, na sekta za fedha bado hazija tengemaa. Tunapoangalia nchi zenye kipato cha juu tunaangalia sana mitaji inayoingia kwa sababu ya fedha zilizopo kwenye uchumi jumla, kuna ukweli kwamba kunakusita katika kuwekeza kwenye nchi zenye uchumi uliojuu kama ulaya, Amerika, na hata Japan na kuwa mtaji mkubwa unaenda kwenye nchi hizo, watu wanaamini kuwa ni hatari kwani kama mlivyoona nchi nyingi tajiri ndio ziliathirika kwa kiasi kikubwa na hivyo

wawekezaji wanahofia kuwekeza fedha zao kwa sababu wanaogopa kuwa chochote kinaweza kutokea kwenye hiyo mitaji yao.Lakini hili tunalifanyia kazi".Alisema Dominique

Sasa, tunajifunza nini kutokana na hili na tunatakiwa tufanye nini huko mbeleni? Wanajimu na wanasiasa wanayajua haya kwahiyo ni wazi kuwa sisi sote tunapaswa kujiweka tayari na kujua jinsi ya kukabiliana na mambo kama haya.alihoji Mkurugrnzi huyo.

Kutokana na jambo hili kutokea lile kundi la nchi 20 linalofuatilia mwenendo wa mabadiliko ya uchumi (G-20 MAP) linajitahidi sana katika kuhakikisha kuwa mambo yote tuliyopangiana wanayafuatilia kwa umakini wa hali ya juu. Kama wote mnavyofahamu kesho ndio tunaanza kuangalia kwa undani zaidi mapendekezo yote yaliyotolewa kuwa yamefikia wapi. Ni kitu kinachohitaji kuendelezwa, kwani ni kwa mara ya kwanza tunafanya lakini najua tutafurahia.

Pili, ni kipindi sasa cha kuleta mabadiliko ya kifedha. Kwa mtazamo wetu katika Shirika la fedha la kimataifa inabidi tukubaliane katika maeneo matatu muhimu mwishoni mwaka huu: Eneo la kwanza,tunaangalia zaidi fedha zilizopo na mitaji, mitaji fedha na mitaji yenyewe; Eneo la pili, tunaangalia ni dhana zipi zitumike ili kukabiliana na hasara zitakazoweza kujitokeza; na tatu; linahusu mpangokazi unaolenga maazimio yote husika.

Pamoja na yote hayo, tunaona kuwa yaliyofanyika katika mambo ya sheria yako sawa na yameenda kwa kasi, lakini kuwe na uangalizi zaidi katika kuzifuatilia sheria hizo.Hii ni muhimu sana. Unaweza ukawa na miongozo mizuri lakini kama haina uangalizi ni kazi bure.Alisema Dominique.

Aidha Dominique alieleza kuwa eneo la tatu linahusiana na tulicho kitengeneza kwa G-20 na mfumo wa Kodi. Nimatumaini yetu kuwa mfumo wa kodi unaweza kusaidia kupunguza mtikisiko ikiwa ni pamoja na sheria zitakazowekwa.

Kodi haziwezi kufanya kila kitu peke yake, sheria nayo ina sehemu yake. Tunacho jaribu kukifanya ni utafiti madhubuti. Katika hili tulijiwekea malengo mawili .Moja ni kupata vitendea kazi ambavyo vitasaidia kuondoa mtikisiko kama upo. Pili, kuwa na dhana ambazo zitasaidia kuondoa au kuzuia hiyo mitikisiko.

Kwa hiyo hayo ndio malengo ya hicho tutakacho kipeleka kwenye majadiliano na G-20.Baada ya hapo itaenda kujadiliwa na Mawaziri wa G-20. Mwisho wakuu wa nchi wataijadili mwezi wa sita.

"Ngoja nimalizie kwa kuwaeleza mambo muhimu na nadhani hamta shangaa kujua kuwa fedha zote zitakuwa mahali pamoja . Kwa hili, jukumu letu linatakiwa liwe zuri zaidi. Hatujaribu kupitia kile kinachofanywa na Shirika la Fedha la kimataifa bali tunataka kuona kuwa tunavyovifanya vinaendana na kinachotakiwa?".aliongeza.

Kwa hiyo, tunataka kuwa wafuatiliaji wa kinachoweza kutokea. Kama mnavyojua, wakati wa mtikisiko, tulijitahidi kuhakikisha tunapandisha dhana ambazo zinaweza kusaidia.Tunajaribu kuweka vitu ambavyo vitasaidia zaidi katika baadhi

ya nchi na nchi.Tuna fanya kazi na nchi mbalimbali ili kusaidia nchi nyingine kuwa na rekodi katika kipindi hiki cha msukosuko.Kwa hiyo tuna mambo mengi tunayoyafanya katika kusaidia nchi wanachama ili kama kutatokea mtikisiko waweze kukabiliana nao kwa kipindi cha miaka miwili, mitano, saba au miaka kumi kuanzia sasa.

Alimalizia kwa kusema kuwa ili yote haya yafanikiwe uongozi unatakiwa ufanye mabadiliko. Na akaahidi kuwa watayatekeleza yale yote waliyokubaliana kule Pittsburgh kwenye mkutano wa G-20 na IMFC. Na kusema kuwa watayafanyia kazi masuala ya viwango vya fedha, suala la upatikanaji wa fedha kwenye uchumi na utumiaji wa fedha hizo unaouwiana na fedha zenyewe.

Mikutano hii ya kimataifa bado inaendelea hapa mjini Washington DC.

Imetolewa na Msemaji Mkuu

Wizara ya Fedha na Uchumi

Washington DC

23/04/2010